**HOTUBA YA MHESHIMIWA JAJI DKT. ELIEZER MBUKI FELESHI, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KWENYE MKUTANO MKUU WA MAWAKILI WA SERIKALI TAREHE 21 MACHI, 2024 KATIKA UKUMBI WA JAKAYA KIKWETE CONVENTION CENTRE JIJINI DODOMA**

Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mhe. Profesa Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania;

Mhe. Mustapher M. Siyani, Jaji Kiongozi Mahakama Kuu ya Tanzania;

Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb.), Waziri wa Katiba na Sheria;

Mhe. Jenista Joachim Mhagama (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu;

Mhe. Dkt. Festo John Dugange (Mb.), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI);

Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb.), Naibu Waziri wa Fedha;

Mhe. Dkt. Juliana Massabo, Jaji Mfawidhi, Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma na Waheshimiwa Majaji wote mliopo;

Mhe. Rosemary Staki Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;

Wahe. Wanasheria Wakuu wa Serikali Wastaafu mliopo;

Mhe. Edward Kisau Olelekaita (Mb.), Mjumbe wa kamati ya kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria;

Bw. Juma Selemani Mkomi, Katibu Mkuu Utumishi;

Bi. Mary Gaspar Makondo, Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria;

Mhe. Balozi Prof. Kennedy Godfrey Gastorn, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

Mhe. Shaaban Ramadhan Abdalla, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

Bw. Sylvester Antony Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka;

Dkt. Boniphace Nalija Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali;

Bw. Frank Kanyusi Frank, Kabidhi Wasii Mkuu na Afisa Mtendaji Mkuu RITA;

Bw. Onorius John Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria;

Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama;

Mhe. Sylvester Joseph Kainda, Msajili wa Mahakama ya Rufani na Kaimu Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania;

Mhe. Projestus Kahyoza, Kaimu Msajili wa Mahakama Kuu

Kamishna wa Polisi Salum R. Hamduni, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU;

Mhe. Jaji Mathew Pauwa Mhina Mwaimu (Mst.), Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;

Bw. Deus Juma Nyabiri, Makamu wa Rais wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (Tanganyika Law Society) na Wahe. Marais, Wenyeviti na Wakuu wa Vyama vingine vya kitaaluma JMAT, TAMWA, TRJA na TANLAP na wengine mliopo;

Wakuu wa Vyuo, Shule za Sheria, Vyuo vya Mafunzo na Vyuo Vikuu mliopo;

Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Idara, Mawakili wa Serikali wa Mikoa, Wakuu wa Mashtaka wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa Divisheni na Vitengo vya Huduma za Sheria hapa nchini;

Maafisa Sheria na Mawakili wa Serikali wa ngazi mbalimbali mliopo;

Wakuu wa vyombo vya Ulinzi na Usalama wote mliopo;

Viongozi wa Vyama vya Siasa mliopo;

Viongozi wa dini na madhehebu mliopo;

Ndugu Viongozi na Wakuu wa Mashirika ya Umma, Taasisi na Idara za Serikali mliopo;

Ndugu Wanahabari na wageni wote waalikwa mliopo;

Mabibi na Mabwana;

**NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, .........**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Namshukuru mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kufika hapa siku ya leo tunapokutana kwenye Mkutano wa Pili wa Chama chetu. Kama ambavyo viongozi wetu wa dini walivyotuombea, tunamwomba Mungu atuongoze ili tuweze kuanza na kumaliza Mkutano huu salama na kwa mafanikio.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Kwa furaha isiyo na kifani ninakukaribisha sana wewe na wageni wetu wote katika Mkutano huu wa pili wa Chama chetu unaofanyika hapa jijini Dodoma. Ninatoa shukrani za dhati kwa kukubali mwaliko wetu wa kuwa Mgeni Rasmi hasa kwa kuwa ninafahamu wingi wa kazi zako.

Kwa namna ya pekee pia nawashukuru sana viongozi wetu Wakuu kutoka mihimili yote ya Dola kwa kuukubali mwaliko wetu na kuhudhuria pamoja na waalikwa wote kama walivyotambulishwa kwako ambao wameungana nasi katika Mkutano huu. Sina neno zuri zaidi ya kusema **asanteni na tunawashukuru sana.**

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Nampongeza sana Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Balozi Profesa Kennedy Godfrey Gastorn, Menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, uongozi wa mpito wa Chama cha Mawakili wa Serikali na Kamati ya maandalizi pamoja na kamati zake ndogo kwa kufanikisha maandalizi ya Mkutano huu. Napenda kuchukua nafasi hii pia kuwashukuru Mawakili wote wa Serikali waliopo hapa kwa kutenga muda wao na kusafiri kutoka maeneo mbalimbali kuja kushiriki katika Mkutano huu. Niwashukuru sana waajiri wa Mawakili hawa kwa kuwaruhusu kusafiri kutoka katika vituo vyao vya kazi na kugharamia safari zao. Pia, niwashukuru wenyeji wetu wakiongozwa na Mhe. Rosemary Staki Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kwa maandalizi na mapokezi mazuri mliyowapatia wageni wetu. Tumefarijika sana kwa upendo wa dhati mliotuonesha, **Asanteni sana**.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Kama Mlezi wa Chama cha Mawakili wa Serikali na kwa niaba yao naomba kutoa pole kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, familia pamoja na Watanzania wote kutokana na vifo vya wapendwa wetu Hayati Alhaji Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa

Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Hayati Edward Ngoyai Lowasa, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vilivyotokea tarehe 29 Februari, 2024 na tarehe 10 Februari, 2024. Mengi ambayo tungeweza kusema kuhusu viongozi hawa kuhusu utumishi wao uliotukuka kwa Taifa letu yalisemwa kwa kina katika vipindi vya maombolezo na mazishi.

Aidha, mbali na hiyo misiba miwili ya Kitaifa, katika vipindi tofauti kwa Mwaka 2023 na 2024 Chama Chetu nacho kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu kiliondokewa na Wanachama wake Saba (7) ambao ni Wakili Tulimbumi Abel (03.06.2023) ambaye alikuwa Mwanasheria Wizara ya Nishati, Wakili Kharist Luanda (27.07.2023) ambaye alikuwa Mkurugenzi Idara ya Katiba na Ufuatiliaji Haki Wizara ya Katiba na Sheria, Wakili Stella Richard Makali (02.11.2023) ambaye alikuwa Mwanasheria wa Serikali Halmashauri ya Iringa, Wakili Joseph Sebastiani Pande 20.12.2023) ambaye alikuwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Wakili Solomon Lokombeso Lwenge (20.02.2024) ambaye alikuwa Wakili Mfawidhi Ofisi ya Wakili wa Serikali (M) Shinyanga, Wakili Jobu Mwalukosya Andindilile (21.02.2024) aliyekuwa Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga na Wakili Dotto Nyankungu (09.03.2024) aliyekuwa Afisa Sheria Halmashauri ya Nyasa. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awape pumziko la amani viongozi na wapendwa wetu. **Naomba tusimame kwa dakika moja tuwakumbuke Viongozi wetu hawa kwa sala/dua.**

## 2.0 MALENGO YA MKUTANO

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali kwa mwaka huu utajumuisha matukio makuu yafuatayo:

a) mosi, Uzinduzi wa Miongozo na Kamati za Ushauri;
b) pili, Uzinduzi wa Nembo na Tovuti ya Chama cha Mawakili wa Serikali;
c) tatu, Uwasilishaji wa Mada mbalimbali na majadiliano; na
d) nne, Uchaguzi wa viongozi wa Chama cha Mawakili wa Serikali.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Mkutano Mkuu huu ni Jukwaa la kitaaluma la wanasheria walio katika utumishi wa Umma ambalo hufanyika mara moja kila mwaka kwa lengo la kutoa fursa kwa Wanachama wa Chama kujadili masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya Sekta ya Sheria kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 6 ya Kanuni za Chama cha Mawakili wa Serikali kuhusu usimamizi na uendeshaji wake (The Public Bar Association (Management and Organization) Regulations, 2019) zilizochapishwa katika Gazeti la Serikali Namba 589 la mwaka 2019 la tarehe 16 Agosti, 2019, miongoni mwa malengo ya Chama ni kukuza ufanisi wa mfumo wa kisheria katika mambo yanayoathiri huduma za kisheria kwa umma na kufanya utafiti na kujenga uelewa kuhusu maendeleo ya huduma za kisheria kwa umma kwa kujiendeleza kupitia mafunzo n.k. Hivyo, Mkutano huu, pamoja na mambo mengine, utatoa fursa kupitia ajenda zilizopangwa kuwawezesha Wanachama

na Viongozi wao kutathmini mafanikio na changamoto wanazokutana nazo wakati wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku katika taasisi zao, kupatiwa mafunzo yanayohusiana na utoaji wa huduma bora za kisheria na kutatua malalamiko ya kisheria kutoka kwa wadau mbalimbali yakiwemo yale ya wananchi. Ofisi yangu itaendelea kufanya kila linalowezekana ili Chama kifikie matarajio yake kwa mujibu wa sheria.

## 3.0 CHAMA CHA MAWAKILI WA SERIKALI

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Chama cha Mawakili wa Serikali kimeanzishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa matakwa ya Kifungu cha 16A(1) cha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268. Chama hiki kilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 29 Septemba, 2022 kikiwa na jumla ya wanachama wapatao 2,652.

Kwa mujibu wa Aya ya 3(2) ya Hati ya Uanzishwaji wa Daftari la Mawakili wa Serikali ya mwaka 2022 iliyotolewa chini ya vifungu vya 24(3) na 16B vya Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura 268 na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na.583B la tarehe 26 Septemba, 2022, Daftari la Mawakili wa Serikali ndilo pekee lenye taarifa za kundi la Wanachama ambao ni Mawakili wa Serikali wote wenye sifa ya kuwa Wanachama wa Chama hiki. Daftari hili linatunzwa na kupatikana katika kikoa cha https://oagmis.agctz.go.tz na liko wazi kwa upekuzi na rejea ya mtu yeyote.

Aidha, Kanuni ya 4 ya Kanuni za Chama cha Mawakili wa Serikali kuhusu usimamizi na uendeshaji wake (The Public Bar Association (Management and Organization) Regulations, 2019) zilizochapishwa katika Gazeti la Serikali Namba 589 la mwaka 2019 la tarehe 16 Agosti, 2019 inatoa fursa ya kuwepo kwa aina nyingine za Wanachama tofauti na Mawakili wa Serikali wanaofanya kazi kwenye utumishi wa Umma. Aina hizo ni wanachama wa heshima na wanachama wenye mapenzi mema na wanaovutiwa na shughuli zinazofanywa na Chama wanaoomba kuwa sehemu ya wanachama wa Chama hicho. Kwa muktadha huo, Waheshimiwa Majaji na Mahakimu wastaafu, mawakili wabobevu wastaafu na wanataaluma wengine katika Sekta ya Sheria wanaweza pia kuwa wanachama wa Chama hiki baada ya kuridhiwa na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Chama baada ya kutimiza vigezo na taratibu mbalimbali zilizowekwa kwa mujibu wa Kanuni hizo.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Tangu kuzinduliwa kwake, Chama hiki kimepata mafanikio kadhaa:

- Chama kimekuwa daraja muhimu kati ya Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, RITA, OR-TAMISEMI na mamlaka nyingine ambako Wanachama wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria. Hatua hii imesaidia kuwafikishia Wanachama kwa urahisi miongozo mbalimbali inayotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ile inayotolewa

na Mamlaka nyingine zenye dhamana ya kufanya hivyo kuhusiana na upatikanaji wa huduma za kisheria;

- Kuwepo kwa Chama kumeleta jukumu endelevu la Utambuzi na Usajili wa Mawakili wa Serikali katika Daftari la Mawakili wa Serikali kupitia Mfumo wa kidijitali wa Office of Attorney General Management of Information System (OAG-MIS) kupitia Kikoa (Domain/link) cha https://oagmis.agctz.go.tz unahohifadhi Daftari hilo. Daftari linaonesha utambuzi na usajili wa wanasheria wote walio katika Utumishi wa Umma wenye sifa za kutekeleza majukumu ya uanasheria katika Utumishi wa Umma.

  Pamoja na lengo kuu la kuwatambua na kuwasimamia Mawakili wa Serikali, usajili wa Mawakili wa Serikali unawezesha kubaini maeneo wanayofanyia kazi na maeneo yao ya ubobevu ili waweze kutumika katika kutoa huduma za kisheria katika maeneo yanayohitaji huduma zao na kutokutoa mwanya kwa mawakili vishoka kutekeleza majukumu hayo.

  Kufikia tarehe 20 Machi, 2024, idadi ya Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria walioajiriwa katika utumishi wa umma na kusajiliwa katika Daftari la Mawakili wa Serikali ni 3,469. Kati ya hao, 116 ni Mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, 662 ni Mawakili wa Serikali waliopo Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, 125 ni Mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu

wa Serikali, 416 wapo TAMISEMI na 2,150 wapo kwenye Wizara na Taasisi nyingine za Serikali.

Ofisi yangu kwa kushirikiana na Chama cha Mawakili wa Serikali na mamlaka nyingine hatutasita kuwachukulia hatua hata kama zitafedhehesha, viongozi na waajiriwa watakaobanika kuwatumia wanasheria ambao hawajajisajili katika Daftari la Mawakili wa Serikali;

- Kuwepo kwa Chama kumeiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuweka miongozo ya kufuatilia utendaji wao na kuandaa mwongozo wa kutumia wakati wa kuchukua hatua kwa wale wanaokiuka maadili na miiko ya kazi kupitia 'The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Provision of Legal Opinion by State Attorneys and Law Officers in Public Service) Guidelines, G.N. No. 32/2023. Kwa kuzingatia matakwa ya vifungu vya 21(4) na 27(3) vya Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi yangu itajizatiti kuhakikisha kiwango cha uadilifu cha Mawakili wa Serikali kinakuwa cha juu na kuongeza tija na ufanisi katika maendeleo ya Utumishi wao Serikalini katika nyadhifa mbalimbali; na

- Aidha, kufuatia tathmini iliyofanyika kwa kazi zinazofanywa na Wanachama Ofisi yangu imeandaa mwongozo wa ukaguzi utakaowasaidia Maafisa Sheria teule kufanya kaguzi katika

maeneo ya kazi kwa lengo la kubaini na kuchukua hatua dhidi ya Viongozi na Mawakili wa Serikali watakaobainika kutozingatia sheria, miongozo na masharti ya mikataba iliyoingiwa na Serikali katika utekelezaji wa majukumu yao.

Zaidi ya hayo, Ofisi yangu iko katika hatua za mwisho kuufanyia maboresho Mfumo wa OAG–MIS ili kuwawezesha Mawakili wote wa Serikali kutuma taarifa zao moja kwa moja kupitia dirisha litakalokuwepo kwa ajili hiyo, tofauti na sasa ambapo taarifa hizo zinatumwa kwa njia ya barua pepe.

## 4.0 KAULI MBIU

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Kauli mbiu ya Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali mwaka huu ni **"Upatikanaji wa Huduma za Kisheria kwa Wananchi ni Nguzo Muhimu kwa Ustawi wa Jamii".** Kauli mbiu hii inakusudia kuonesha changamoto zilizopo katika sekta ya sheria na kutukumbusha wanachama kwamba, wakati wa utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku, tunawajibika kuhakikisha kila tunalolifanya, daima linalenga kuwahudumia wananchi kwa weledi na uadilifu mkubwa ili kuendeleza amani na utulivu katika nchi yetu na hivyo kuchochea ustawi wa jamii yetu.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Kauli Mbiu ya Mkutano huu inakikumbusha Chama hiki na Mawakili wa Serikali kuhusu jukumu lao na Serikali kwa ujumla kuhakikisha wananchi wa

Tanzania ambao ndio msingi wa mamlaka yote wanawezeshwa kustawi. Ibara ya 8(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatamka kwamba:

> **"Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii, na kwa hiyo –**
>
> **(a) wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii;**
>
> **(b) lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi;**
>
> **(c) Serikali itawajibika kwa wananchi; na**
>
> **(d) wananchi watashiriki katika shughuli za Serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.**

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Tarehe 13 Machi, 2024, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Tanzania alisitiza wajibu huo mara baada ya kuwaapisha Wakuu wa Mikoa na Naibu Katibu Mkuu. Katika hafla hiyo, pamoja na mambo mengine, Mhe. Rais alizungumzia juu ya malalamiko ya Wananchi ambayo bado ni mengi. Hivyo, ni wajibu wetu kuwatumikia wananchi waliotupatia dhamana ya kufanya kazi hizi kwa niaba na kwa ajili yao kupitia utumishi huu wa umma huku lengo kuu likiwa ni ustawi wa wananchi dhima ambayo imekuwa sehemu ya Kauli Mbiu ya Mkutano wetu Mkuu wa Mawakili wa Serikali kwa Mwaka huu wa 2024.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Kauli mbiu hiyo inatutaka kujitathmini ni kwa namna gani tunawawezesha wananchi kupata huduma za kisheria na kuchochea Ustawi wa Jamii. Natambua kuwa sisi Mawakili wa Serikali tunawajibika kutoa huduma za kisheria kwa Serikali na tumekuwa na mchango mkubwa kupitia huduma hizo kwa Serikali na Taasisi zake ambazo zipo kuwahudumia wananchi. Hata hivyo, miongoni mwa changamoto kubwa zinazoendelea kutukabili ni kukosekana kwa mfumo endelevu wa kutoa huduma za kisheria kwa wananchi wenye malalamiko dhidi ya Serikali na taasisi zake, kutotambulika kwa taasisi zinazotoa huduma za kisheria kwa wananchi, wananchi kutopatiwa huduma za kisheria kwa wakati na wananchi kutojua mahali sahihi pa kupeleka malalamiko yao ili kupata huduma za kisheria.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Aliyekuwa rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali nchini Georgia (State Bar of Georgia) Patrise M. Perkins–Hooker wakati akitoa hotuba yake ya ukaribisho tarehe 7 Juni, 2014 katika Mkutano wa Chama hicho alisema maneno yafuatayo, ninanukuu:

> **"The practice of law is not a right. It is a privilege! Along with this privilege, comes a moral obligation to ensure that all the citizens of this great state have reasonable access to legal services. Those of us honored with the privilege have a duty and a responsibility to make sure that everyone has access to a lawyer when coming into court. No one should lack access to**

**valuable legal services during the most vulnerable times of their lives".**

Kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba:

**"kazi ya utoaji wa huduma ya kisheria sio haki. Ni upendeleo! Sambamba na huu upendeleo, linakuja jukumu ambata la kimaadili la kuhakikisha wananchi wa Taifa hili kubwa wanao uwezo wa kuzifikia huduma za kisheria. Kwa wale tuliopata heshima hiyo tuna jukumu na wajibu wa kuhakikisha kwamba kila mtu anaweza kumpata mwanasheria anapokuja mahakamani. Asiwepo mtu atakayekosa kupata huduma stahiki za kisheria anapozihitaji katika nyakati ngumu na muhimu maishani."**

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Nukuu ya maneno ya Mwanasheria Msomi na rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali nchini Georgia (State Bar of Georgia) Patrise M. Perkins–Hooker hapo juu inashabihiana na Kanuni ya 4 ya Kanuni za Msingi za Umoja wa Mataifa kuhusu Majukumu ya Wanasheria (Principle 4 of the UN Basic Principles on the Role of Lawyers) za mwaka 1990 inayosomeka ifuatavyo, nanukuu:

**"Governments and professional associations of lawyers shall promote programmes to inform the public about their rights and duties under the law and the important role of lawyers in**

**protecting their fundamental freedoms. Special attention should be given to assisting the poor and other disadvantaged persons so as to enable them to assert their rights and where necessary call upon the assistance of lawyers."**

Kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba, ninanukuu:

**"Serikali na vyama vya kitaaluma vya wanasheria watahamasisha uwepo wa programu za kuutaarifu Umma kuhusu haki na wajibu walionao kwa mujibu wa sheria pamoja na jukumu muhimu la wanasheria katika kulinda uhuru wao wa kimsingi. Mkazo maalum utapaswa kuwekwa katika kuwasaidia maskini na watu wenye uhitaji wa kipekee ili kuwawezesha kudai haki zao na inapolazimika, kuomba msaada wa wanasheria."**

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Ni ukweli usiopingika kwamba, kwa kuwa idadi kubwa ya wananchi wetu, kwa sababu moja au nyingine bado wanakwenda mahakamani bila kuwakilishwa na mawakili, Chama cha Mawakili wa Serikali kama ilivyo kwa Serikali, Mahakama, Chama cha Mawakili Tanganyika na wadau wengine, kama ilivyobainishwa na hata kwa mtizamo wa kidunia hapo juu, wote kwa pamoja wanao wajibu wa kuweka mikakati endelevu ya kutekeleza Kauli Mbiu ya Mkutano huu ambayo ni "**Upatikanaji wa Huduma za Kisheria kwa Wananchi ni Nguzo Muhimu kwa Ustawi wa Jamii".** Hii itawezekana kwa kuhakikisha huduma za kisheria zinapatikana kwa wananchi bila upendeleo,

kwa gharama nafuu au bila gharama yoyote hususan kwa wananchi wasio na uwezo.

## 5.0 NAMNA YA KUTEKELEZA KAULI MBIU

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Nimeeleza awali kwamba kila Wakili wa Serikali ambaye ni mwanachama wa Chama cha Mawakili wa Serikali ana wajibu wa msingi wa kutoa huduma za kisheria kwa Serikali na Taasisi zake ambazo zipo kuwahudumia wananchi. Majukumu ya Wakili wa Serikali yamefungamanishwa na Usajili wake na Uanachama wake kama inavyoainishwa katika Aya ya 6 ya Hati ya Uanzishwaji wa Daftari la Mawakili wa Serikali ya Mwaka 2022 inayosomeka, nanukuu:

> **"6.-(1) Wanasheria wote walioingizwa katika Daftari la Mawakili watakuwa Mawakili wa Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 24(3) cha Sheria na kwa kuzingatia masharti ya aya ndogo ya (2), watakuwa na haki ya kuhudhuria na kusikilizwa katika mahakama zote za Jamhuri ya Muungano.**
>
> **(2) Pamoja na majukumu mengine yaliyoainishwa na Sheria nyingine yoyote, Mawakili wa Serikali watakuwa pia na uwezo wa-**
>
> **(a) kutoa ushauri kwenye masuala ya kisheria ikiwa ni pamoja na masuala yanayohusu uhakiki wa mikataba kwa kuzingatia miongozo iliyotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**

**(b) kushiriki katika uandishi wa sheria na hati mbalimbali za kisheria kwa kuzingatia mwongozo na maelekezo ya Mwandishi Mkuu wa Sheria;**

**(c) kuendesha mashauri ya jinai baada ya kupewa hati maalum ya kukasimiwa madaraka hayo na Mkurugenzi wa Mashtaka;**

**(d) kuendesha mashauri ya madai baada ya kupewa hati maalum ya kukasimiwa madaraka hayo na Wakili Mkuu wa Serikali;**

**(e) kushiriki katika majadiliano kwa niaba ya Serikali baada ya kuteuliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**

**(f) kutoa huduma za kuthibitisha nyaraka na kushuhudia viapo kwa mujibu wa Sheria husika; na**

**(g) kutekeleza jukumu lingine lolote kama takavyoelekezwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali."**

Bila kuathiri masharti ya Katiba, sheria, miongozo na Kanuni zinazomtaka Mwanachama wa Chama cha Mawakili wa Serikali kutekeleza majukumu yake kwa Serikali na taasisi anakofanya kazi, Chama kinayo fursa ya kutekeleza Kauli Mbiu ya mwaka huu na kuhakikisha Wanachama wanawekewa utaratibu wa kutoa huduma za kisheria kwa wananchi kwa kushirikiana na wadau na kuleta amani, mshikamano na ustawi katika Jamii kupitia njia zifuatazo:

- **Kutoa Ushauri wa kisheria** katika masuala mbalimbali yanayolalamikiwa na wananchi yenye asili ya kisheria mahali pa kazi kupitia uratibu wa Madawati ya Malalamiko yaliyopo au kwa kuanzisha Dawati Maalum la kutoa Ushauri wa Kisheria papo kwa hapo kama ilivyo ofisini kwangu kupitia simu maalumu ya bure namba **0800 110 188** ambapo mamlaka za Serikali na wananchi wanawasiliana moja kwa moja. Vilevile, huduma hii inapatikana kupitia mfumo wa kieletroniki. Aidha, mfumo wa Call Center na Mrejesho wa Huduma kwa Mteja (Feedback) unaotumika mahakamani unaweza kuigwa na taasisi wanakofanyia kazi Wanachama.

  Nitoe wito kwa Idara, Kurugenzi na Vitengo vya Huduma za Sheria katika Wizara na taasisi za Serikali kuweka ratiba za kuwasikiliza wananchi wenye malalamiko dhidi ya Serikali wanaofika katika maeneo yao na hata kuwafuata katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kutoa ushauri wa kisheria kwa wananchi hao. Chama ngazi ya Mkoa na mahali pengine kutenga siku za Chama cha Mawakili wa Serikali au kwa kushirikiana na wadau wengine kutoa msaada wa kisheria bure (*Pro bono publico)* kwa Umma;

- Aidha, njia nyingine ni Chama kwa uratibu wa Wizara ya Katiba na Sheria kutoa Msaada na Huduma za kisheria ngazi ya Mkoa kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (*Mama*

*Samia Legal Aid Campaign)* ambayo uliizindua tarehe 27 Aprili, 2023 hapa Jijini Dodoma;

- **Chama kuendelea kutoa Elimu kwa umma kuhusu maeneo yenye changamoto za kisheria.** Utekelezaji wa zoezi hili ni kupitia Wanachama wa Chama cha Mawakili wa Serikali. Elimu hiyo iendelee kutolewa kupitia vyombo vya habari zikiwemo televisheni, redio, magazeti, miongozo, semina na vipeperushi. Njia hii imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwani imewasaidia wananchi wanaopata elimu hiyo kujua mahali sahihi pa kupeleka malalamiko yao; na

- **Kuanzisha vituo jumuishi elekezi na wezeshi** kwa kuwashirikisha wadau wote kwenye mnyororo wa utoaji haki kwa lengo la kuwapokea wananchi wengi wasiojua mahali sahihi pa kupeleka migogoro yao ya kisheria na kuwasikiliza. Vituo hivi kama nilivyoeleza mara tu baada ya  kutembelea mabanda ya wadau katika Wiki ya Sheria Jijini Dodoma tarehe 28 Februari, 2024 na kuirudia Siku ya Sheria tarehe 1 Februari, 2024 vitajikita zaidi kujua mwananchi anayefika mbele ya wadau hao ana mgogoro gani, je umeshashughulikiwa na kama bado ni mamlaka ipi inapaswa kuushughulikia? Je, kama ni mgogoro binafsi, anao uwezo wa kuweka Wakili na kisha kumpatia usaidizi unaoendana na majibu ambapo wadau watatumia fursa ya kuwa pamoja kuhakikisha migogoro hiyo inashughulikiwa na mamlaka stahiki

ambapo watatumia mifumo kupata mrejesho. Hatua hii pia itadhibiti mawakili vishoka na wananchi wanaotapeli wananchi wenzao.

## 6.0 CHANGAMOTO

**Mheshimiwa Waziri Mkuu;**

Ili kutekeleza kwa mafanikio tarajiwa lengo la Chama cha Mawakili wa Serikali na Wanachama wake kwa kuwapatia huduma za kisheria wananchi kuendana na Kauli mbiu ya Mwaka huu, ninayo heshima kubwa kuiomba Serikali kushughulikia changamoto zifuatazo:

### 6.1 Ajira

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara na Taasisi za Serikali bado zinakabiliwa na upungufu wa watumishi hususan Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria. Kwa mujibu wa sheria, kwa mfano, wakati Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inapaswa kuwa na Mawakili wa Serikali mpaka ngazi ya Wilaya, Ofisi yangu na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa upande mwingine zinapaswa kuwa na Mawakili wa Serikali mpaka ngazi ya Mkoa. Upungufu uliopo sasa kwa mfano, umeifanya Ofisi yangu kuwa na Ofisi katika Mikoa kumi tu hivyo kuathiri utendaji kazi. Hivyo, tunaiomba Serikali kuendelea kutoa vibali vya kuajiri Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria katika taasisi zake ili kuboresha utoaji wa huduma za sheria Serikalini pamoja na kufanya

utekelezaji wa Kauli Mbiu ya Mwaka huu kwa matarajio yaliyoelezwa hapa awali.

## 6.2 Vitendea Kazi

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na hata Taasisi za Serikali wanakofanya kazi Mawakili wa Serikali bado zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa vitendea kazi hususan vyombo vya usafiri na kompyuta ambazo ni nyenzo muhimu za kuwawezesha kutekeleza majukumu ya kila siku. Namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia Kompyuta Mpakato (Laptop) 150 ikiwa ni utekelezaji wa ahadi yake aliyoitoa wakati akizindua Chama cha Mawakili wa Serikali tarehe 22 Septemba, 2022.

Kwa kuwa tatizo hili linaendelea kutukabili naiomba Serikali iendelee kuangalia uwezekano wa kuzipatia Ofisi Kuu za Sheria nilizozitaja walau Kompyuta 300 na kuwaelekeza waajiri wote OR-TAMISEMI, Wizara na Taasisi kumpatia kila Wakili na Afisa Sheria kompyuta.

Aidha, kwa kuwa Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali ngazi ya Mikoa zote hazina nyenzo za usafiri, naiomba Serikali walau iiwezeshe kununua au kupewa magari 12 kwa kuanzia na kupata magari mengine kwa ajili ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ngazi ya Wilaya.

## 6.3 Maslahi ya Mawakili Wa Serikali

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaendelea kufanya maboresho ya maslahi ya Watumishi wa umma. Nitumie fursa hii kuwafahamisha kuwa, kwa mujibu wa Kifungu cha 8(3)(d) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 8A(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298, tarehe 20 Septemba, 2023 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitoa Waraka wa idhini ya malipo ya posho na stahili za Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria wanaotekeleza majukumu yao katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi za Umma, Wakala wa Serikali na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Kwa Waraka huo, kuanzia tarehe 1 Julai, 2024, Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria wanapaswa kulipwa posho na ada mbalimbali ikiwemo posho ya vazi maalum kwa Mawakili (Court Attire Allowance), posho ya usaidizi wa pango (Rent Housing allowance), ada ya Chama cha Mawakili wa Tanzania Bara (TLS), ada ya Kamishna wa Viapo wa Mahakama Kuu na zile za chini yake kwa Mawakili walioapishwa, ada ya Chama cha Mawakili wa Serikali (TPBA) na posho ya simu kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Waraka huo.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Nitumie nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja

na  mamlaka husika kwa kuridhia ongezeko hilo la posho kwa Mawakili wa Serikali. Hata hivyo, kwa kuzingatia mazingira ya kipekee ya kazi na miiko ya Wakili wa Serikali ambao wao kama walivyo Waheshimiwa Majaji na Mahakimu, tofauti na baadhi ya taaluma ambazo hutumia muda wao wa ziada kujiongezea kipato, ninaomba tena kadri hali ya Uchumi wetu itakavyoruhusu, kuwaongezea mishahara na maslahi yao ili ziendane na hali halisi ya sasa ya kiuchumi nchini. Aidha, Watendaji Wakuu  wa taasisi za umma washauriwe kuwalipa Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria madeni yao kwa wakati ikiwemo malimbikizo ya mishahara na mafao ya wanasheria wastaafu ili kuepusha malalamiko na kushusha morali ya utendaji kazi kwa Mawakili hao.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Kwa kuwa Chama hiki kinalelewa na Serikali kupitia kwa Mhe. Rais na alishatoa maelekezo kwamba kiwezeshwe na Serikali kulipia mafunzo, ada za Uanachama katika vyama vya kitaaluma, posho nyingine stahiki pamoja na upandishwaji wa madaraja naomba kuwasilisha kwako ombi la kuweka msisitizo kwa mamlaka za ajira kutoa kipaumbele katika kutekeleza maelekezo ya Mhe. Rais wanapokutana na mazingira hayo.

## 6.4 Ujenzi wa Vituo Jumuishi vya Utoaji Haki

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Mojawapo ya changamoto zinazosababisha wananchi wengi kushindwa kufikia huduma za kisheria ni umbali wa vituo vya kutolea huduma. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, ninaiomba Serikali iendelee kuutafutia fedha Mpango wa Serikali kujenga majengo yatakayokuwa Vituo Jumuishi na

kutumiwa na Taasisi zote za Serikali zinazotoa huduma za kisheria (Government Legal Institutions Integrated Centers–GLIICs) ambao ulianza mwaka wa fedha 2021/2022 katika mikoa ya Mwanza na Arusha kupitia Fungu 16 na kwa mikoa ya Pwani, Morogoro, Ilala (Kinyerezi), Katavi, Rukwa, Mbeya, Manyara, Njombe, Geita na Shinyanga kupitia Fungu 35.

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Kwa kuwa Sehemu ya Tano ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inahimiza kudumisha uongozi na utawala wa kisheria, Serikali inatakiwa kujenga uwezo wa sekta ya umma, taasisi za kijamii, vyombo vya Habari, Bunge, taasisi za kusimamia sheria na taasisi zote za ndani na nje ya dola zinazochochea uwajibikaji na kutetea matakwa ya jamii. Dira hii inachochea Serikali kuwekeza rasilimali zake katika maeneo ya msingi yatakayotuwezesha kufikia malengo ya maendeleo na inahimiza wananchi kushirikishwa katika programu mbalimbali za maendeleo. Chama hiki na Mawakili wa Serikali wataungana kama Taifa kufanikisha utekelezaji wa lengo hilo kupitia Dira hii inayofika ukomo ifikapo mwakani, yaani, mwaka 2025 pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022–2025/2026 ambao shabaha yetu ni kujenga Ofisi 10 za Mikoa kupitia Mpango wa GLIICs.

## 7. USHIRIKIANO NA SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa njia ya

kubadilishana mawazo na uzoefu unaolenga kuboresha huduma zinazotolewa na Ofisi hizi. Katika Ofisi yangu, masuala yanayoihusu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yanashughulikiwa na Dawati Maalum ambalo limeanzishwa mahsusi kwa lengo la kuratibu ushirikiano baina ya Ofisi hizi mbili katika maeneo mbalimbali ikiwemo, utoaji wa ushauri wa kisheria, uandishi wa Sheria na Mikataba n.k. Katika kutekeleza mashirikiano hayo, wapo baadhi ya watumishi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar walioletwa ofisini kwangu kwa lengo la kujifunza namna tunavyofanya kazi.

## 8. MIONGOZO

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Katika Mkutano wa Mawakili wa Serikali uliopita uliofanyika Septemba, 2022 nilieleza kuwa, Ofisi yangu inaendelea kuandaa Miongozo mbalimbali itakayowasaidia Mawakili wa Serikali ambao ninawajibika kuwasimamia katika kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa Majukumu yao ya kila siku. Miongozo mipya ambayo imeboreshwa na imeandaliwa na kukamilika na ambayo utatuzindulia ni hii ifuatayo:

a) Mwongozo wa Utengenezaji wa Sheria Ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa;
b) Mwongozo wa Uandishi wa Sheria (Legislative Drafting Manual);
c) Mwongozo wa Mikataba (Contract Manual);
d) Mwongozo wa Utoaji wa Ushauri wa Kisheria;
e) Mwongozo wa Kamati za Ushauri wa Kisheria Ngazi ya Mkoa na Wilaya;

f) Istilahi za Sheria; na
g) Majina ya Sheria kwa Lugha ya Kiswahili.

Kwa heshima na taadhima, tunakuomba baada ya hotuba yako utuzindulie miongozo hiyo ili ianze kutumika rasmi. Pia, tunakuomba utuzindulie Nembo ya Chama cha Mawakili wa Serikali pamoja na tovuti ya Chama cha Mawakili wa Serikali ambayo itarahisisha mawasiliano baina ya wanachama kwa njia ya kidijitali.

## 9. KAMATI ZA USHAURI

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Kama nilivyodokeza hapo juu, Mwongozo wa Kamati za Ushauri wa Kisheria Ngazi ya Mkoa na Wilaya ni miongoni mwa Miongozo utakayoizindua leo. Mwongozo huu pamoja na mambo mengine umeanzisha Kamati ambazo zitaundwa na Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria walio katika maeneo yao ya kazi. Kamati hizo zimepewa jukumu la kutoa ushauri wa kisheria na kusikiliza malalamiko yanayoihusu Serikali kutoka kwa wananchi bila malipo kwa kushirikiana na Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya husika. Hii itasaidia kuwa na jukwaa endelevu la Serikali katika kusikiliza malalamiko ya wananchi nje ya mfumo wa Mahakama na hivyo kuokoa muda na gharama ambazo mwananchi angezitumia kupeleka malalamiko yake mahakamani.

Aidha, kwa kuwa wananchi wataokoa muda ambao wangetumia kwenda mahakamani ambako mashauri huchukua muda mrefu, watapata muda zaidi wa kujishughulisha na shughuli za kujitafutia kipato na hivyo kuwa na jamii

yenye ustawi bora. Vievile, jukwaa hilo litawasaidia wananchi kutohangaika kutafuta haki sehemu zisizo sahihi ambako hupoteza muda mwingi au hata kupoteza haki zao kutokana na kuzitafuta sehemu isiyo sahihi. Hii ni kwa sababu wananchi hawa watapata huduma au miongozo sahihi ya kisheria kutoka kwa Mawakili wetu wa Serikali watakaokuwa wakipatikana huko. Ni imani yangu kuwa wananchi watajitokeza kwa wingi kutumia fursa ya uwepo wa Kamati hizo katika maeneo yao na kupokea huduma stahiki ipasavyo.

Ni mategemeo ya Ofisi yangu kuwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya husika watatoa ushirikiano wa kutosha kwa Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria walio katika maeneo yao ya kazi ili waweze kutekeleza jukumu hili ipasavyo. Nitumie pia nafasi hii kukuomba Mhe. Waziri Mkuu utuzindulie Kamati hizo leo ili zianze rasmi utekelezaji wa jukumu hilo muhimu.

## 10. UCHAGUZI WA VIONGOZI WA CHAMA CHA MAWAKILI WA SERIKALI

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Chama cha Mawakili wa Serikali kilichozinduliwa tarehe 22 Septemba, 2022 na Mhe. Rais kinaongozwa na viongozi wa mpito ambao ni:

a) Wakili Michael Marcellus Luena–Rais;
b) Wakili Lucas Charles Malunde–Makamu wa Rais;
c) Wakili Stephano Seba Mbutu–Mwenyekiti;
d) Wakili Hassan Mayunga–Makamu mwenyekiti;
e) Wakili Sia Beatrice Mrema–Katibu; na
f) Wakili Irene Joseph Lesulie–Mweka hazina.

Tangu Chama cha Meawakili wa Serikali Tanzania (Tanzania Public Bar Association–PBA) kilipozinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 29 Septemba, 2022, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria viongozi wa mpito wa Chama hicho wamefanikiwa kufanya mambo mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) Kukutana na uongozi wa Chama cha Mawakili wa Kujitegemea (Tanganyika Law Society–TLS) kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali yanayohusu wanachama wa Chama cha Mawakili wa Serikali ambao pia ni wanachama wa TLS ikiwemo kukubaliana viwango vya ada wanazopaswa kulipa kila mwaka;

(b) Chama cha Mawakili wa Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kilikamilisha usajili wa kikoa (domain) cha Chama na kufungua akaunti ya benki. Pia, Chama kinalo Sanduku la Posta, anuani ya barua pepe pamoja na tovuti kwa ajili ya mawasiliano na taarifa;

(c) Uongozi wa mpito wa Chama cha Mawakili wa Serikali ulishiriki katika Wiki ya Sheria jijini Dodoma;

(d) Uongozi ulikutana na Uongozi wa Wizara ya Katiba na Sheria;

(e) Uongozi unaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa Kampeni ya Mama Samia Legal Aid inayoendelea kutekelezwa nchi nzima;

(f) Wataalam wa TEHAMA kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, TLS na eGA walikutana kwa ajili ya kuoanisha (harmonize) mfumo wa TLS–Wakili Data Base na OAG–MIS; na

(g) Uongozi wa mpito wa Chama pia umefanikiwa kuandaa na kukamilisha Kanuni za Uchaguzi wa viongozi wa Chama cha Mawakili wa Serikali, Miongozo na Standard Operating Procedures (SOPs).

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Nitoe pongezi kwa uongozi wa mpito wa Chama cha Mawakili wa Serikali ambao umekiongoza Chama hiki tangu kilipozinduliwa rasmi na Mhe. Rais na wanatarajia kumaliza muda wao siku ya kesho tarehe 22 Machi, 2024 ambapo Mkutano Maalum wa Uchaguzi wa Viongozi wa Chama utafanyika. Ni matumaini yangu kuwa Viongozi watakaochaguliwa watasaidia kuwahimiza wanachama wa Chama cha Mawakili wa Serikali kuendeleza juhudi za utoaji wa huduma za kisheria kwa wananchi na Serikali kwa ujumla. Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kisheria unafikia zaidi ya asilimia 90% ya wananchi wote nchini. Nitoe rai kwa Mawakili wenzangu wa Serikali kupigania upatikanaji wa huduma za kisheria kwa wananchi bila kuchoka.

## 11. **HITIMISHO**

**Mheshimiwa Waziri Mkuu**

Napenda kumalizia hotuba yangu kwa kuiomba Serikali iendelee kuweka mkazo katika kuhakikisha inatuwezesha kutimiza jukumu hili kwa

ufanisi na ufasaha. Ni dhahiri kuwa sisi kama Mawakili wa Serikali tunapenda kuona malalamiko na kero za wananchi zinatatuliwa.

Baada ya hayo, naomba sasa nimkaribishe Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, Waziri wa Katiba na Sheria ili aweze kusema machache kisha akukaribishe Mheshimiwa Mgeni Rasmi ili uongee na hadhara hii ambayo ina shauku ya kukusikiliza.



Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**

**21 Machi, 2024**